

## BOARD OF TRUSTEES

**WARD A** Sherri O'Keefe  
**WARD B** Marsha Nelson  
**WARD C** Marcia Hole  
**WARD D** Trisha Estabrooks  
**WARD E** Dawn Hancock  
**WARD F** Julie Kusiek  
**WARD G** Saadiq Sumar  
**WARD H** *vacant*  
**WARD I** Jan Sawyer

## SUPERINTENDENT OF SCHOOLS

Darrel Robertson  
  
Centre for Education  
1 Kingsway NW  
Edmonton AB T5H 4G9  
**T** 780-429-8000  
**F** 780-429-8318  
**E** info@epsb.ca

Tarehe 7 Juni, 2023

Kwa familia, wazazi na walezi,

Katika majira ya mapukutiko ya mwaka wa 2022, Shule za Umma za Edmonton zilifanya utafiti kati ya wanafunzi ili kupata maelezo zaidi kuhusu wanafunzi tunaowahudumia. Wanafunzi katika Gredi za 4 hadi 12 walipata fursa ya kushiriki maelezo kuhusu wao wenyewe. Maswali kwenye utafiti yaligusia mambo yafuatayo:

- Utambulisho wa asili
- utambulisho wa rangi
- kabila
- mwelekeo wa kidini au kiroho
- utambulisho wa kijinsia
- mwelekeo wa kijinsia (Gredi za 7 hadi 12 tu)

Ushiriki katika utafiti ulikuwa wa hiari kabisa. Wazazi ambao hawakutaka mtoto wao kushiriki wangeweza kuondoa mtoto wao. Wanafunzi walioshiriki katika utafiti huu walijibu tu maswali waliyohisi wakiwa huru kujibu.

**Asante!**

Zaidi ya wanafunzi 55,800 walijibu utafiti huo, ambao ni kiwango cha majibu cha asilimia 73. Ningependa kuwashukuru wanafunzi ambao walichukua muda wa kukamilisha utafiti. Tunashukuru sana kwa nia yao ya kushiriki maelezo yao wenyewe. Tuna fahari kwamba wanafunzi katika shule zetu ni wa kutoka asili mbalimbali, tamaduni, jamii na uzoefu.

**Matokeo ya utafiti**

Matokeo ya awali ya utafiti sasa yanapatikana mtandaoni, pamoja na taarifa mpya na video mpya. Ninakuhimiza kutembelea [tovuti yetu](#) ili kusoma ripoti na kupata maelezo zaidi kuhusu hatua zetu zinazofuata katika kazi hii.

**Tukiendelea mbele**

Shule za Umma za Edmonton zimejitolea kufanya kazi kwa makusudi ya kupambana na ubaguzi wa rangi, upatanisho na usawa kupitia hatua za kuendelea, kujifunza na kuboresha. Katika miaka ijayo, matokeo ya utafiti yatajumuishwa na maelezo mengine ya mwanafunzi ili kuelewa vizuri hali ya wanafunzi katika shule na pale ambapo Idara inaweza kuchukua hatua ili kupunguza viziuzi. Kupitia kazi hii nia yetu ni kuchukua hatua ambazo zinalenga wakati ujao ambapo wanafunzi wote wanaweza kujivunia hali yao, kuhisi huru na kupata mafanikio shuleni.

Wenu Mwaminifu,



Darrel Robertson  
Msimamizi wa Shule